PELUM KENYA

# TOLEO MAARUFU YA
# SERA YA KITAIFA YA MAZINGIRA (2012)

Kulingana na Usimamizi wa Mazingira na Sheria ya Uratibu-EMCA (1999), Sheria ya Misitu(2005), Sheria ya Maji (2002) na Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Wanyama Pori (2009)

Imetayarishwa na:
**Elmard Omollo**
The International Development Institute-Africa (IDIA)

Septemba, 2013

UKaid from the British people

EMBASSY OF SWEDEN
Nairobi

Act!

Hati miliki 2013
Chama  Shirikishi Ekolojia Matumizi na Usimamizi wa Ardhi  (PELUM) Kenya, Haki zote zimehifadhiwa.

Habari, takwimu, tarifa na vielelezo kutoka machapisho haya ni hati miliki ya PELUM Kenya, na inaruhusiwa kutumika kwa ajili ya mandishi inayoelekeza maendeleo au kwa madhumuni ya elimu inayotolewa na kusambazwa bure bila malipo iwapo PELUM Kenya na wandishi  wake watatambuliwa.

Nilazima Taarifa za Kiufundi zilizotolewa kuthibitishwa kabisa iwezekanavyo kwani PELUM Kenya haitakubali dhima.
Maoni yaliyotolewa hapa si lazima kueleza maoni ya wahariri au PELUM Kenya.

**Timu ya wahariri wa PELUM Kenya**

**Maryleen Micheni**
Afisa mwandamizi wa Mradi, Utafiti na Usimamizi wa habari

**Teklah Majuma**
Msaidizi wa Mradi

**Shukrani**
Humphrey Mwambeo, Diana Njihia, Jeff Kahuho, Ann Majani, Zachary Makanya,
PELUM Kenya na Act! CRM kituo

PELUM KENYA

# Toleo Maarufu

**Ya**

# Sera ya Kitaifa ya Mazingira (2012)

Kulingana na Usimamizi wa Mazingira na Sheria ya Uratibu-EMCA (1999), Sheria ya Misitu(2005), Sheria ya Maji (2002) na Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Wanyama Pori (2009)

Imetayarishwa na

**Elmard Omollo**
The International Development Institute-Africa (IDIA)

**Yaliyomo** **Ukurasa**


1.0 Utangulizi .......... 5

2.0 Katiba Na Mchango Wa Umma .......... 6

3.0 Faida Za Kuushirikisha Umma .......... 9

4.0 Tunawezaje Kuhifadhi Mazingira Yetu? .......... 9

5.0 Kanuni Za Sera Ya Kitaifa Ya Mazingira .......... 11

6.0 Mchango Wa Jamii Katika Usimamizi Wa Mazingira .......... 12

6.1 Misitu .......... 12

6.2 Mito Na Maziwa .......... 13

6.3 Milima .......... 14

6.4 Sehemu Kame Na Kavu .......... 16

6.5 Ardhi .......... 17

6.6 Udongo .......... 18

6.7 Wanyama Pori .......... 20

6.8 Wanawake Na Mazingira .......... 21

6.9 Vijana Na Mazingira .......... 23

## 1.0 UTANGULIZI

Mazingira ni neno linalojumuisha sehemu zinazozingira maeneo ya makazi na ya kufanyia kazi - pawe ni ofisini, barabarani, kitongojini, ziwani, baharini au hata msituni. Katika Mazingira yoyote yale, kila Mkenya ana haki yakuwa na mazingira yanayoimarisha afya, safi na salama na yenye kuzuia uchafuzi na uharibifu. Wakenya wote hutegemea moja kwa moja au vinginevyo bidhaa na huduma zinazotolewa na mazingira. Huduma na bidhaa hizi ni kama vile kuni, maji kwa matumizi ya nyumbani, wanyama pori ambao huzalisha mapato ya kigeni kwa kuwavutia watalii, miti na misitu inayovutia mvua na hivyo kuboresha uzalishaji wa kilimo, maziwa, bahari, na mito ya kuvua samaki na kutupatia umeme kwa matumizi ya viwandani. Kwa hivyo, raslimali ya mazingira yetu huchangia moja kwa moja na vinginevyo katika ukuzaji wa uchumi wa taifa kwa kukuza mapato na uzalishaji wa mali. Kwa hiyo, mazingira safi na yenye kuboresha afya siyo tu haki kwenye Katiba ya Kenya (2010) bali pia ni kiungo muhimu katika kufikia malengo ya maendeleo ya Kenya kwenye mpango wa Dira 2030.

Tangu Kenya inyakue uhuru mwaka wa 1963, Taifa limeweza kuchukuwa hatua kubwa za kimaendeleo ambazo zimechangia pakubwa katika uharibifu wa mazingira kwa sababu ya mbinu mbovu za ukulima, ukosefu wa mbinu mwafaka za kuhifadhi udongo na maji, ukataji miti (ukataji haramu wa miti au 'kufyeka na kuchoma'- binu ya kilimo), ufugaji unaopita kiasi na uchafuzi wa mazingira. Uharibifu wa mazingira yetu umechangia kuongezeka kwa gharama ya kuyafanya maji kuwa salama, kuongezaka kwa bei ya chakula na matibabu hospitalini. Ili kukabiliana na ongezeko la changamoto za mazingira, Serikali – kwa njia ya kushirikisha umma imeendeleza sera ya mazingira (2012) ambayo inataka miongoni mwa mengine:

a) Kuimarisha mchango wa umma katika kufanya maamuzi kama njia moja inayohitajika kwa ajili ya maendeleo endelevu.
b) Kuzuia na kudhibiti aina za viumbe hai ambazo zinatishia mazingira, mimea, na wanyama wanaoishi humu kwa mfano gugu maji na magugu aina ya Mathenge
c) Kuanzisha mazingira ya pamoja (misitu, wanyama pori, ardhi nyevu, maji safi) katika uhifadhi wa raslimali za asili kwa sababu ya uhusiano uliopo na shughuli kuu za kiuchumi kwa mfano misitu iliyoko milimani ni vyanzo vikuu vya mito ambayo huzalisha nguvu za umeme na pia ni makao ya wanyama wa pori ambao huwavutia watalii.
d) Kuzingatia na kudhibiti viwango vya umasikini ambavyo huweka shinikizo kwenye mazingira kwa sababu ya kukosa njia mbadala. Kwa mfano ukataji haramu wa miti na kuchoma makaa ili kukidhi mahitaji ya familia.

e) Kutungwa kwa sheria kali na adhabu dhidi ya mtu yeyote anayeharibu mazingira na pia kuboresha utekelezaji wa sera za mazingira.

f) Kurejesha (pengine kwa hali ya awali) maeneo ambayo yameharibiwa na kurudisha uhai wa viumbe hai (aina za mimea na wanyama) uliopotea. Kwa mfano, bidii za kupanda tena miti katika Msitu wa Mau na kuondolewa kwa gugu maji katika Ziwa Victoria zafaa kuungwa mkono na kutiliwa mkazo.

## 2.0 KATIBA NA MCHANGO WA UMMA

Ushirikishi wa raia ni mchakato wa njia mbili ambapo serikali inatoa fursa kwa ushirikishi wa umma na pale ambapo umma huchagua ikiwa watatumia fursa hizo kulingana na kiwango cha uhusika, umuhimu na habari waliyonayo. Sheria muhimu ya nchi, katiba ya Kenya (2010) imeutaka umma kushiriki katika uundaji wa sera, usimamizi wa mazingira, na ugavi na matumizi ya rasilimali za umma kama ifuatavyo:

1. Kila Mkenya ana haki ya mazingira safi na yenye kuimarisha afya lakini umma pia una wajibu wa kulinda na kuhifadhi mazingira. Mkenya yeyote (binafsi au kwenye kikundi) anaweza kuenda mahakamani wakati haki hizi zimekiukwa, na serikali au na watu wengine.
2. Katiba inahitaji serikali kuhifadhi misitu ya kitaifa kwa asilimia kumi (kwa sasa misitu inakadiriwa kuwa asilimia 2.3 ya taifa), ina maana kwamba bidii ya Wakenya na Serikali inahitajika kwa jumla ili kuifanya kuwa asilimia kumi.
3. Serikali ina wajibu wa kuhimiza ushirikishi wa umma katika usimamizi na uhifadhi wa mazingira [Ibara ya 69 (1) (d)].
4. Bunge linahitajika kuidhinisha matumizi yoyote ya rasilimali asili za Kenya na kwa hivyo lafaa kuhusishwa kikamilifu katika majadiliano ya mikataba inayohusiana na matumizi ya madini ya taifa, mafuta, makaa ya mawe, mazao ya misitu na wanyama pori. Hapa, mchango wa umma ni kupitia wabunge waliochaguliwa kidemokrasia nao wanaopaswa kuwajibikia wanaowawakilisha.
5. Ibara ya 56 inapendekeza uwakilishi wa walio wachache na makundi yaliyotengwa (wanawake, vijana na walio wachache) ambao kiasili walitengwa katika maamuzi ya kijamii na serikali. Kwa mfano, mchango wa kabila la Ogiek katika msitu wa Mau na pia kabila la Endorois katika rasilimali za ziwa Bogoria umetambuliwa hivi majuzi baada ya kampeni za kijamii ndani na nje ya mahakama.




6. Katiba inaunga mkono upatikanaji wa habari ambazo zinahakikisha ushirikishi fanisi wa umma. Bunge la taifa na Mabunge ya kaunti yanatakiwa kuandaa mikutano hadharani na kuendeleza shughuli zao machoni mwa umma. Katika Ibara ya 35, wananchi wana haki ya kupata habari zote kutoka kwa serikali na mashirika yake. Hii ni muhimu haswa kwa leseni za Tathmini ya Athari za Mazingira (IEA) ambazo hutolewa katika mazingira yenye utata.

**SERA YA MAZINGIRA YA TAIFA (2012) INAHIMIZA USHIRIKISHI WA MAKUNDI YA WALIO WACHACHE KATIKA UHIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**



## 3.0 FAIDA ZA KUUSHIRIKISHA UMMA

Kuna faida nyingi zinazotokana na kuushirikisha umma.Mifano ni pamoja na:

- Maafisa wa serikali wanaweza kuelewa na kukabiliana vizuri na mahitaji ya jamii zao
- Kuongezeka kwa maafikiano (makubaliano ya mawazo) kati ya maafisa wa serikali na jamii juu ya maswala muhimu na utoaji wa huduma
- Jamii zinaarifika vyema juu ya miswada ya kuhifadhi na kusimamia mazingira inayoendelezwa na mashirika ya serikali kwa mfano Shirika la Kitaifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMA), Huduma za Misitu ya Kenya (KFS), Huduma za Wanyama Pori (KWS) na Shirika la Usimamizi wa rasilmali ya maji (WRMA) miongoni mwa mengine.
- Maswala yanayohusu Jamii yanamakiniwa na kupewa kipaumbele ili kushugulikiwa na maafisa wa serikali. Mfano ni Mchakato wa Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA) ambapo maoni ya umma hukaribishwa na kuzingatiwa kabla ya NEMA kuruhusu mradi wowote wa maendeleo.
- Wananchi wanafahamu vyema jinsi serikali inagawa na kutumia pesa za umma na hivyo kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa raslimali za umma.
- Ushirikishi wa umma kupitia kwa muamko na elimu ya mazingira huongeza uwezo wa umma kuheshimu sheria, maagizo na kanuni za uhifadhi wa mazingira. Kama matokeo tutashuhudia kesi za ukataji miti haramu na watu kujenga makao misituni, kuuawa kwa wanyama pori, mizozo ya binadamu na wanyama wa pori na uharibifu wa mito na maziwa yatapungua kwa kiasi kikubwa.

## 4.0 TUNAWEZAJE KUHIFADHI MAZINGIRA YETU?

- Kukataza upandaji wa miti ya Mikaratusi karibu na mito, mabwawa au maziwa
- Kuhimiza sheria ya “6-R” katika usimamizi wa taka Kataa(Refuse), Kupunguza( Reduction), Kurudisha(Return), Kujaza(Refill), Marudio( Reuse), na Kusaga( Recycle).
- Kutohimiza uchimbaji mitaro katika machimbo ya madini ili kuepuka uharibifu wa mali na kupoteza maisha
- Kusafisha mito
- Kuepuka ufugaji zaidi ya kiwango kilichowekwa
- Kujenga muundo unaomwezesha mkulima kukuza mimea katika mazingira anayopendelea “greenhouses” kulingana

**JAMII INA HAKI YA MAZINGIRA SAFI NA YENYE KUBORESHA AFYA, PAMOJA NA JUKUMU LA KULINDA NA KUBORESHA HAYO MAZINGIRA.**



na sheria husika

- Kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira(EIA) kabla ya kuanza shughuli kuu ya kiuchumi kama inavyohitajika na sheria
- Kuharamisha shughuli za kilimo katika maeneo ya uhamaji ya wanyama ili kupunguza mizozo kati ya binadamu na wanyama pori
- Kupunguza mmomonyoko wa udongo kwa kutumia njia sahihi za kilimo kwa mfano kuchimba matuta na mbinu nyingine zakuzuia mmonyoko wa udongo "gabions"
- Kupitisha kilimo hai (organic farming) ili kupunguza uchafuzi unaotokana na mbolea za kemikali na madawa ya kuua wadudu
- Kulinda ardhi inayopakana na maeneo ya maji na kupanda mimea kwenye ardhi iliyo tupu
- Kuharamisha kilimo kwenye maeneo yanayopakana na barabara au reli
- Kuhimiza uvunaji wa maji shambani

## 5.0 KANUNI ZA SERA YA KITAIFA YA MAZINGIRA

Miongoni mwa nyingine, Sera ya Mazingira (2012) itatekelezwa kwa mujibu wa kanuni elekezi zifuatazo:

- Ushirikishi wa Umma: mbinu shirikishi kwa usimamizi na ulinzi wa mazingira itakuzwa ili kuhakikisha kuwa serikali za taifa na Kaunti, mashirika husika ya serikali, sekta binafsi, vyama vya kiraia na jamii zimehusishwa katika kupanga, kutekeleza na kufanya maamuzi.
- Haki ya Mazingira Safi na yenye kuimarisha afya: Kila Mkenya ana haki ya mazingira safi na yenye kuimarisha afya, haki inayoandamana na jukumu la kuhifadhi na kuboresha ubora wa mazingira. Hivyo, Wakenya wanahimizwa kutotupa taka katika maeneo ya umma, kutoelekeza ghafi ya maji taka katika vyanzo vya maji (mito na maziwa), kutokata misitu ili kujenga makao au ukulima na uuaji wa wanyama pori katika maeneo yaliyolifadhiwa (mbuga za wanyama na maeneo hifadhi).
- Kanuni ya Ugamvi Mamlaka: usimamizi wa mazingira na rasilimali za kiasili utahamishwa kutoka kwango cha kitaifa na kuhamishwa katika mchakato wa ugatuzi hadi kiwango cha chini zaidi. Matukio haya yafaa kuungwa mkono na vyama vya misitu ya jamii (CFA's), Bodi ya Ardhi ya Jamii (CLB's) na kamati za usaru wa maeneo anzishi (catchment area).
- Kanuni za tahadhari: pale ambapo kuna vitisho vikali au uharibifu wa kudumu kwa rasilmali muhimu za mazingira, ukosefu wa dhibitisho sahihi ya kisayansi hautakua msingi wa sababu ya kutokataza uendelezi wa uharibifu huo wa

mazingira. Kwa mfano, samaki katika Mto Mara wanakufa kwa tarakimu kubwa, NEMA yaweza kusimamisha utoaji wa takataka (salama /si salama) kwenye mto huku shughuli za kubaini chanzo cha uchafuzi zikiendelea.

- Usawa Katika Kizazi na baina ya vizazi: usimamizi wa mazingira na rasilmali za asili utafanywa kwa kuzingatia maoni ya muda mrefu huku chaguo la kizazi cha leo cha wakenya kikifaidi bila ya kupunguza uwezo wa vizazi vya baadaye (watoto na wajukuu wetu ) kukidhi matakwa yao.

## 6.0 MCHANGO WA JAMII KATIKA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

### 6.1 Misitu

Kwa mujibu wa Sera ya Mazingira ya Taifa (2012), maeneo yenye misitu ya Kenya imepungua kwa haraka kutokana na mbinu duni za kilimo kwa mfano, kukata miti kwa sababu ya ukulima na uzalishaji wa chakula na makazi ya jamii, uzalishaji wa viwanda, uchomaji wa makaa na maendeleo ya miundo mbinu( kwa mfano ujenzi wa barabara). Changamoto nyingine ni pamoja na ukataji haramu wa miti kwa ajili ya kuni na malisho ya mifugo misituni. Hata hivyo kiwango kikubwa cha kupungua kwa misitu kimesababisha hasara kama kupungua kwa mazao ya kilimo, mvua imekuwa haba na isiyotabirika na kukauka kwa mito, uzalishaji wa viwanda umepungua na majanga makubwa ya kiasili ( kama vile mafuriko na ukame). Miongoni wa mambo mengine serikali imependekeza:

1. Kuongeza maeneo yenye misitu na miti kwa angalau asilimia kumi (10%)
2. Kulinda na kuhifadhi misitu ambayo ni vyanzo vikuu vya mito na maji
3. Kusaidia utekelezaji wa sera ya Misitu na sheria

**Ushirikishi Wa Jamii Katika Uhifadhi Na Usimamizi Wa Misitu**

- Sera ya Misitu imebuni Sheria ya Misitu (2005). Sheria nayo inabuni Huduma za Misitu ya Kenya (KFS) ambayo inasimamiwa na bodi ambayo inawakilisha jamii za msituni miongoni mwa washika dau wengine.
- Sheria ya Misitu imeanzisha Vyama vya Misitu vya Kijamii (CFAs), Pia imezipa jamii za karibu haki ya kutumia, kufikia na kudhibiti rasilmali za misitu. Pia hutoa nafasi kwa ajili ya usajili wa Vyama vya Misitu vya Kijamii (CFA's) chini ya sheria ya Vyama (Societies Act). Chama Cha Msitu cha Kijamii (CFA) kilichosajiliwa kinaweza kumuomba mkurugenzi wa

Huduma za Misitu ya Kenya (KFS) ruhusa ya kushiriki katika uhifadhi na usimamizi wa misitu ya umma.

- Huduma za Misitu ya Kenya (KFS) ina madaraka ya kuanzisha maeneo hifadhi ya misitu ambayo yatasimamiwa chini ya Kamati Hifadhi ya Misitu (FCCs). Kamati hizi zinajumuisha watu wanne wenye ujuzi wa misitu na ambao wameteuliwa na Vyama vya Misitu vya Kijamii (CFA's) ambazo zinafanya kazi katika maeneo hayo.
- Ili kuhakikisha matumizi endelevu ya misitu kwa ajili ya kuchoma makaa, Kanuni ya Misitu ya 2009 inawahitaji wanabiashara wanaochoma makaa kujipanga kama makundi ya kibiashara au mashirika ya wachoma makaa ili kuhakikisha kuchoma makaa endelevu na wanachama wake.
- Huduma za Misitu ya Kenya (KFS) inahitaji kupitisha mfumo wa mashauriano katika kuunda mipango ya vuguvugu la misitu ya umma (PFM) kwa kutafuta maoni ya jamii na serikali za kaunti zinazofaidi kutokana na misitu.
- Sheria pia inapendekeza fedha za kutumika kwa uhifadhi wa Misitu ya kiasilia, kuunga mkono misitu ya kijamii miongoni mwa mambo mengine. Hivyo basi pesa zinazoundwa kutokana na uhifadhi wa misitu zitarudishwa kwa jamii.

## 6.2 Mito na Maziwa

Kwa mujibu wa Sera ya Mazingira ya Taifa(2012), maeneo ambayo yana maji safi na sehemu za ardhi zenye unyevu (kwa mfano mabwawa) ni muhimu katika utoaji wa maji safi ya kunywa, sehemu za kuwanywesha wanyama maji na pia ukuzaji wa mimea kama vile,mihogo, mchele, na mboga. Kenya imetia saini Mkataba wa Ramsar(Rasmar convention) na hivyo inahitajika kutambua na kuhifadhi ardhi nyevu zenye umuhimu wa kimataifa (Ramsar Sites). Hizi ni pamoja na: Maziwa Nakuru, Naivasha, Baringo, Bogoria, Elementeita na Tana Delta. Hata hivyo, sehemu hizi zinazidi kuharibiwa na shughuli za kibinadamu. Ili kukabiliana na hali hiyo, serikali itachukua hatua zifuatazo:-

1. Kuunda na kutekeleza mikakati ya pamoja ya usimamizi wa ardhi nyevu na raslimali ya maji
2. Malipo kwa miradi ya huduma ya kimazingira ili kuunga mkono uhifadhi wa raslimali ya maji
3. Kuunda na kutekeleza sera na sheria za ardhi nyevu za kitaifa
4. Kuratibu majukumu ya mashirika mbalimbali yanayosimamia raslimali za maji safi na ardhi nyevu

**Ushirikishi wa jamii katika usimamizi wa maji safi**

- Kamati ya Ushauri ya Maeneo yenye vyanzo (CAAC) ambayo imejumuishwa na washika dau wa raslimali hutoa ushauri katika ngazi za chini mitaani kuhusu matumizi, usimamizi na uhifadhi wa raslimali ya maji.
- Mkakati wa Usimamizi wa vyanzo (CMS) hutoa njia za kuziwezesha jamii kushiriki katika usimamizi wa raslimali ya maji katika maeneo yao kupitia kamati za ushauri wa vyanzo vya maji chini ya sheria ya maji (2002).
- Vyama vya Haki za wanaotumia Maji (WRUAs) vinaundwa kama vikao vya ushirikiano katika usimamizi wa raslimali ya maji na pia kusuluhisha migogoro inayotokana na matumizi ya raslimali hii. Vikundi hivi vinaundwa na wanaotumia raslimali ya maji.
- Sheria imeanzisha Mfuko wa Huduma ya Maji (WSTF) ambao lengo lake kuu ni kusaidia katika ufadhili wa miradi ya maji katika maeneo ambayo hayajashugulikiwa vya kutosha hususani katika mitaa yenye maskini na vijijini.
- Bodi ya Rufaa ya Maji inatoa njia ambayo wanaotumia maji wanaweza kutumia kutafuta haki wanapodhulumiwa na maamuzi, ya moja kwa moja au katika nyanja tofauti, yanayotolewa na taasisi za sekta ya maji.
- Kanuni ya Usimamizi na Uratibu wa Mazingira 2009 ( ardhi nyevu, kando za mito, kando za Maziwa na Bahari) inaunga mkono elimu, ubunifu, na vitendo vya jamii za karibu pamoja na maisha ya jadi ambayo yanahusika katika uhifadhi na uendelezi wa aina za mimea na miti.

## 6.3 Milima

Sera ya Mazingira ya Taifa (2012) imetambua maeneo yenye milima kuwa muhimu katika uhifadhi wa aina za mimea na wanyama. Milima pia huvutia mvua na pia ndio vyanzo vya maji kwa mfano vyanzo vya mito mingi huwa ni maeneo ya milima kama Mlima Kenya, Mlima Elgon, Milima ya Aberdare, Ngome ya Mau na Vilima vya Cherengani. Hata hivyo maeneo ya milima yamehatarishwa kwa matumizi yenye madhara kama vile ukataji haramu wa miti, uuaji na wizi wa wanyama pori na mimea, uharibifu kutokana na moto na uchimbaji wa madini, ulishaji wa mifugo usiothibitika, makazi haramu ya binadamu, kilimo cha mimea na madhara ya mabadiliko ya hewa.

Serekali itafanya haya:

1. Kufanya utafiti utakaoongeza maarifa ya kutumia maeneo ya milima kwa ufanisi
2. Kukuza shughuli mbadala za kuzalisha mapato kama njia ya kuboresha ushirikishi wa jamii katika uhifadhi wa maeneo yenye milima

## UHIFADHI WA MAJI NA UDONGO HUSABABISHA MAZAO BORA YA MIMEA NA WANYAMA



3. Kupitisha matumizi na mipango ya ardhi inayofaa na usimamizi wa tengamaji ili kuhakikisha ukuzaji endelevu wa maeneo ya milima

**Ushirikishi wa jamii katika Kusimamia maeneo ya Milima**

- Chini ya Sera ya Taifa ya Mazingira (2012), serikali imejitoa kuunga mkono taratibu mbadala na pia kushirikisha umma katika kuhifadhi uhai wa milimani.
- Chini ya Sheria ya Misitu (2005), maeneo ya milima yanaweza kusimamiwa na Jumuiya ya Vyama Msitu (CFAs). Mashirika ambayo yamepewa nguvu kushirikiana Na Huduma ya Misitu ya Kenya katika kuendeleza mipango ya ushirikiano kwa usimamizi wa misitu.
- Maelekezo Jumuishi ya matumizi ya ardhi (2009) inataka :
    - Kuhimiza kilimo cha mseto katika ardhi iliyo kwenye milima. Hata hivyo aina yoyote ya ukulima katika maeneo ya mteremko kati ya asilimia 12% - 55% lazima izingatie hatua mwafaka za kudhibiti udongo na maji.
    - Kuendeleza upatikanaji na faida za taratibu za ugavi kwa kuzingatia misitu, bidhaa zinazotokana na wanyama pori na uzalishaji wa mapato.
    - Chini ya Usimamizi wa Mazingira na Sheria ya Uratibu - 1999 (EMCA), kila kamati ya mazingira wilayani (sasa Kaunti) ina nguvu kuhimiza upandaji wa miti katika maeneo ya milimani kupitia kwa shughuli hiari za kusaidia katika maeneo ya jamii.

## 6.4 Sehemu Kame na Kavu

Kwa mujibu wa Sera ya Mazingira ya Taifa (2012), sehemu Kame na Kavu (ASALs) hupokea mvua haba ambayo haitabiriki. Sehemu kubwa ya ardhi katika maeneo kame na kavu inatumika kwa ufugaji. wafugaji katika maeneo kame na kavu huenda kutoka sehemu moja hadi nyingine wakitafuta maji na malisho ambayo yanamilikiwa na jamii kwa pamoja na husimamiwa na jamii.

**Serikali inapendekeza:**

1) Kuendeleza na kutekeleza mpango wa pamoja wa matumizi ya ardhi kame na kavu (ASALs)
2) Kuhakikisha usimamizi wa pamoja wa raslimali ya maji katika sehemu kame kwa lengo la kuvuna maji ya mafuriko na ya

mvua

3) Kutekeleza mpango wa utekelezaji wa taifa (NAP) ili kupunguza kuenea kwa jangwa na kutilia nguvu mfuko wa pesa zitakazo fadhili mikakati ya kupambana na kuenea kwa jangwa (Desertification Trust Fund)

**Ushirikishi wa Jamii Katika Usimamizi wa Sehemu Kame na Kavu**

- Sera ya Ardhi inabainisha kuwa wafugaji wanakosa uwakilishaji, hivyo kufanya haki zao za ardhi kupuuzwa na hivyo inahimiza serikali kuweza kuwashirikisha wafugaji kwenye maaumizi juu ya ardhi na raslimali zinazohusisha ardhi.
- Sera ya kitaifa ya Usalama wa Chakula na Lishe (2012) inakuza upana wa ushirikishi wa washika dau pamoja na jukumu kubwa la sekta binafsi, masoko, vyama vya kiraia na jamii za karibu katika awamu zote na hivyo kufanya usalama wa chakula jukumu la taifa zima.
- Huduma ya Misitu ya Kenya inaendelea kukuza misitu kwenye ardhi kavu kama njia ya kurejesha ubora wa mazingira katika sehemu Kame na kavu. Kwa hivyo, ushirikishi wa jamii kupitia Vyama vya Misitu vya Kijamii (CFAs) unahimizwa.
- Katiba ya Kenya (2010) na Sera ya Taifa ya Ardhi (2009) zinahimiza matumizi ya njia mbadala za kusuluhisha mizozo ya raslimali na hili ni muhimu katika sehemu Kame na Sehemu kavu kule ambako ufugaji ndio shughuli kuu ya kiuchumi

## 6.5 Ardhi

Kwa mujibu wa Sera ya Mazingira ya Taifa (2012), ardhi ni adimu, yenye uwezo wa kuibua hisia na isiyo rejelezi; hata hivyo mazao ya ardhi yanaweza kuboreshwa, kwa mfano kwa kutumia mbolea ya wanyama. Ardhi ni mali ambayo hutumika kupokea mikopo kutoka kwa benki ili kupanua biashara, mijengo, na huduma muhimu katika kuboresha maisha ya binadamu. Kama matokeo uhitaji na shinikizo kwa ardhi vinaongezeka kila uchao kwa sababu ya kuongezeka kwa idadi ya watu; hivyo basi mahitaji ya chakula na makazi yanaongezeka. Shughuli zinazopunguza ubora wa ardhi ni pamoja na: mbinu duni za ukulima, udongo dhaifu na shughuli duni za usimamizi wa maji, kumaliza misitu, ufugaji unaozidi kiwango na janga za kiasili ( pamoja na mafuriko na maporomoko ya ardhi). Serikali imeahidi kutekeleza Sura ya Tano ya Katiba ya Kenya ( 2010) inayohusu ardhi, Sera ya Ardhi ( 2009), na Sera ya Mazingira ya Taifa( 2012) ili kuboresha ubora wa ardhi kwa manufaa ya Wakenya wote.

**Ushirikishi wa jamii katika usimamizi wa Ardhi**

- Sera ya Kitaifa ya Ardhi inapelekea serikali kujitoa kuunda sheria zinazotambua haki za jamii katika matumizi ya raslimali za ardhi rejelezi na zile zisio rejelezi katika kuleta utumizi endelezi wa raslimali kwa jamii.
- Chini ya Sera ya Kitaifa ya Ardhi, serikali itaweka sheria na njia za utawala kwa ajili ya kuamua na kugawa faida zinazopatikana kutokana na raslimali asili ya jamii.
- Sera ya Kitaifa ya Ardhi, inapelekea serikali kuunda taasisi tatu muhimu za usimamizi wa ardhi. Baadhi yao - Tume ya Kitaifa ya Ardhi, Bodi ya Ardhi Wilayani, na Bodi ya Ardhi ya Jamii. Bodi hizi za Wilayani na Jamii zitakuwa na wawakilishi wa jamii waliochaguliwa kidemokrasia wanaojumuisha ngazi za chini zaidi za usimamizi na utawala gatuzi wa ardhi.
- Sera ya Ardhi inaelekeza serikali kuanzisha taasisi tatu muhimu za usimamizi wa ardhi: Tume ya Ardhi ya Taifa (NLC), Bodi ya Ardhi ya Wilaya (DLBs) na Bodi ya Ardhi ya Jamii (CLBs). Bodi ya Ardhi ya Wilaya (DLBs) na Bodi ya Ardhi ya Jamii (CLBs) zitajumuisha wawakilishi waliochaguliwa kidemokrasia, na kuunda ngazi ya chini ya ugatuzi ya utawala na usimamizi wa ardhi
- Bodi ya Ardhi ya Wilaya (DLBs) na Bodi ya Ardhi ya Jamii (CLBs) zinahimizwa kutumia mikakati Mbadala ya utatuzi wa migogoro kama vile upatanishi, usuluhishi ili kuwezesha haki na kupatikana haki katika maswala ya ardhi
- Sera ya Kitaifa ya Ardhi inapelekea serikali kujitoa kuhakikisha kutambuliwa rasmi kwa maarifa asili kuhusu raslimali za ardhi na kutoa mifumo ya uendelezo na utumizi wa maarifa asili.
- Kurejesha ubora wa mazingira ya ardhi, Sera ya Kitaifa ya Ardhi inaelekeza serikali kuhimiza matumizi ya njia asili za kuhifadhi ardhi.

## 6.6 Udongo

Udongo wenye rutuba ni muhimu katika ukulima wa mimea. Udongo pia ni muhimu katika kudhibiti mitiririko ya maji. Upungufu wa miti na nyika umepunguza mimea kwenye ardhi na kuchangia mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na upepo katika maeneo mengi ya Taifa. Idadi ya wakulima wanaotumia mbolea ili kuboresha mavuno yao hata ingawa njia hii huharibu ubora wa ardhi ya kilimo. Kwa mujibu wa Sera ya Mazingira ya Taifa (2012), serikali itaanzisha Mpango wa Taifa wa kuhifadhi udongo, kukuza kilimo hai ili kudumisha rutuba ya udongo, kuhakikisha ulinzi wa ardhi nyevu, kingo za mito, na miteremko kutokana na shughuli zenye madhara ili kuzuilia mmomonyoko wa udongo na uharibifu wa mazingira.

**SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA URATIBU (1999) INAHITAJI TATHMINI YA ATHARI YA MAZINGIRA KABLA YA MRADI WOWOTE WA MAENDELEO KUANZA. WANAJAMII WANATARAJIWA KUTOA MAONI YAO.**



**Ushirikishi wa jamii katika uhifadhi na usimamizi wa udongo**

- Usimamizi wa Mazingira na Sheria ya Uratibu -EMCA ya 1999 inatoa uhifadhi na urejeshi wa ardhi nyevu, kingo za mito, juu ya milima, na miteremko kupitia kwa kamati za wilaya/ kaunti za mazingira ambazo zinajumuisha wawakilishi wa jamii za wakulima au wafugaji, makundi yasiyo ya kiserekali, na wanabiashara.
- Miongozo ya kitaifa ya uvunaji mchanga (2007), huunda kamati za kiufundi za kuvuna mchanga zitakazo jumuishwa na watu kutoka kwa kamati za wilaya/ kaunti za mazingira na wanajamii watakaochaguliwa ili kuzingatia shughuli za kuvuna mchanga katika kaunti.
- Miongozo ya kuvuna mchanga pia huunda Vyama vya utunzaji wa raslimali zilizo kando ya mito (Riparian Resource Management Associations) zinazoundwa na kamati za kaunti za mazingira zinazo jumuishwa na wanachama watakaochaguliwa kutoka kwa jamii husika ili kuwajibika katika usimamizi endelevu wa kuvuna mchanga katika eneo la shughuli zake.
- Kamati ya Kaunti ya Mazingira ina jukumu la kudhibiti shughuli zote katika ardhi nyevu (kama vile kusimamia utengenezaji wa matofali, uvunaji wa mchanga na udongo, wanaotumia wakihitajika kuunda mashirika ya kujitolea na panapohitajika wapewe leseni kulingana na Usimamizi wa Mazingira na Sheria ya Uratibu -EMCA ( Kanuni za Ardhi nyevu ) ya 2009.

## 6.7 Wanyama Pori

Kwa mujibu wa Sera ya Mazingira ya Taifa (2012), wanyama pori huchangia moja kwa moja na vinginevyo katika uzalishaji wa mapato katika ngazi za chini na kitaifa haswa kutokana na utalii wa kigeni na pia kutajirisha. Hata hivyo, kuongezeka kwa idadi ya watu, migogoro kati ya binadamu na wanyama pori, mauaji na wizi wa wanyama na mimea iliyohifadhiwa, uchafuzi wa mazingira, kubadilika kwa hali ya anga na kubadilishwa kwa maeneo wanaoishi wanyama pori kuwa ardhi za ukulima au makazi, zote zimechangia kupungua kwa idadi ya wanyama katika mbuga za wanyama pori. Serikali inapendekeza:

1. Kulinda, kuhifadhi, na kuongeza maeneo ya wanyama pori na njia za uhamiaji.
2. Kufaidisha uwekezaji katika utalii na shughuli za uhifadhi na ulinzi wa mimea na wanyama pori.
3. Kuhimiza na kuunga mkono uanzishaji wa maeneo ya uhifadhi ya kijamii ili kuongeza nafasi ya wanyama pori.
4. Kuunga mkono mashirika kama Huduma za Wanyama Pori (KWS) katika utafiti na usimamizi ili kupata taarifa ya kutosha kufanya maamuzi

**Ushirikishi wa jamii katika uhifadhi na usimamizi wa Wanyama pori**

Sera ya Kitaifa ya Uhifadhi na Usimamizi wa Wanyama Pori (2012) inatoa:

- Ugatuzi wa usimamizi wa wanyama pori hadi ngazi za chini zaidi kwa kuunga mkono ushirika wa sekta binafsi, mashirika yasio ya kisirekali na makundi ya kijamii (CBOs);
- Kuhimiza ushirikishi wa jamii katika uhifadhi na usimamizi wa wanyama pori kupitia kuanzishwa kwa maeneo ya uhifadhi wa wanyamapori kwenye jamii, na usimamizi wa pamoja wa Maeneo yaliyohifadhiwa.
- Kufunzwa kwa jamii, kamati za kaunti za kuhifadhi wanyama pori, na mashirika ya wanyama pori yaliyosajiliwa ili kusimamia na kuhifadhi wanyama pori na kubadilisha fikira baina ya wanajamii, mashule, na vikundi vingine husika na pia kupunguza uharibifu wa mimea, wanyama na upotezaji wa maisha ya binadamu.
- Kutengeneza muundo madhubuti wa kugawa faida ikiwa ni pamoja na mapato ya jamii zinazoishi pamoja katika eneo la hifadhi la wanyama na maeneo mengine yaliyohifadhiwa.
- Kuchagua njia wanyama pori wanaotumia kuhama na maeneo ya kusambaa kwa kuhusisha jamii pamoja na miradi ya ubunifu kama vile miradi ya kuwezesha uhamaj,i"easements" mazingira na mikataba ya usimamizi.
- Kukuza utumizi wa maarifa ya asili katika uhifadhi na usimamizi wa raslimali ya wanyama pori.
- Kukuza ushirikiano kati ya jamii na sekta binafsi kwenye biashara ya wanyama pori zenye faida ili kukuza uzalishaji wa mapato na kuinua kiwango cha maisha vijijini.

Sheria ya Wanyama Pori (Uhifadhi na Usimamizi) inamruhusu mkurugenzi wa Shirika la Wanyama Pori la Kenya kuteua kutoka miongoni mwa wananchi walinzi wa heshima (honorary guards) ili kusaidia Shirika hili katika kutekeleza mamlaka yake chini ya Sheria.

## 6.8 Wanawake na Mazingira

Wanawake wanaingiliana na mazingira katika shughuli zao za kila siku wanapolima mashamba, kukusanya kuni na kuchota maji. Kwa mujibu wa Sera ya Mazingira, serikali inajitolea katika kulainisha maswala ya jinsia katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira na raslimali za kiasili.

**JINSIA INA JUKUMU KUBWA KATIKA USIMAMIZI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA.**



Usimamizi wa Mazingira na Sheria ya Uratibu -EMCA (1999) zinahusisha wawakilishi wa wanawake katika kamati za mazingira zilizo wilayani (kaunti) kama mojawapo ya mipango ya serikali katika kuhusisha wanawake katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

## 6.9 Vijana na Mazingira

- Vijana wanajumuisha zaida ya asilimia 50% ya wakazi wa nchi. Hivyo basi ni muhimu kushirikisha vijana na kuhakikisha kuwa mahita ji yao maalum yanaangaziwa na kushughulikiwa kwa lengo la kukuza usimamizi endelevu wa mazingira.
- Kulingana na Sera ya Mazingira, serikali inajitolea kujumuisha maswala ya vijana katika usimamizi wa mazingira sawa na kuendeleza na kufanyisha kazi Mkakati wa vijana na Mazingira na Mpango wa Utekelezaji .
- Usimamizi wa Mazingira na Sheria ya Uratibu -EMCA (1999) inajumuishwa na vijana wawakilishi kwenye kamati za mazingira zilizo kwenye mikoa na wilaya (Kaunti).
- Chini ya Mpango wa Utekelezaji wa Hali ya Hewa wa Kitaifa 2013-2017, serikali itachukua hatua kuboresha hali ya hewa na Mipango ya Maandalizi ya Janga itakayofanywa na makundi ya jinsia zote; pia kuna hitaji la kuwawezesha vijana na wanawake.

## KUHUSU PELUM KENYA

- Chama Shirikishi Ekolojia Matumizi na Usimamizi wa Ardhi (PELUM) ni mtandao wa mashirika ya kiraia /na Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi na wakulima wadogo wadogo wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini. Shirika hili huwezesha Kusoma, Kuungana, na Kutetea usimamizi endelevu wa raslimali asili kwa ajili ya maisha bora. Wanachama wake wamejumuishwa kutoka kwa mashirika yasiyo ya Kiserikali, Mashirika ya Kidini, Asasi za Kijamii na Makundi ya Kiraia ambayo kwa sasa imesimamia mungano wa mashirika 42.
- PELUM ina maono ya jamii yenye uwezo na yaliyofaulu katika kukidhi matakwa yao ya maisha kwa matumizi endelevu ya ardhi. Shirika hili lina juhudi za kukuza ushirikiano katika matumizi na usimamizi wa shughuli za ardhi kwa ajili ya kukuza maisha ya wakulima wadogo wa Kenya kupitia mbinu za ushirikiano katika matumizi na usimamizi wa mazingira ya ardhi.

Mungano wa PELUM Kenya una juhudi za:

- Kuinua ushirikiano katika matumizi na shughuli za usimamizi wa ardhi hapa Kenya
- Kuimarisha uwezo wa taasisi za mtandao wake na wanachama husika
- Kukuza miungano, kujuzana, na upashanaji wa habari, kati ya wanachama wake
- Kukusanya tajiriba ya uzoefu wa maendeleo kwa kuunganisha maarifa ya kiufundi ya kiasili na kusambaza kwa walengwa
- Kutetea na kushawishi shughuli endelevu na sera zinazofaa kwa manufaa ya wakulima wadogo.

**PELUM Kenya**
P.O Box 6123 – 01000, Thika, Kenya
SACDEP Training Centre, Upper hill road next to Central Memorial Hospital
Tel: +254 20 26 22 674 Fax: +254 20 26 22 674
Email:pelumkenya@pelum.net
www.pelum.net

**Kubuni na Mpangilio**
Urban Wave Designs
Tel: 020 2323758
Mobile: 0734 723288
Email: urbanwavedesigns@gmail.com

**Michoro**
Henry Kissinger
Cell: 0722 911 967
Email: henryopati@yahoo.com